KISWAHILI GREDI YA 9

MUHULA WA 1 2026

MUDA: SAA 2 DAKIKA 30

JINA……

<u>SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)</u>

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Katika karne hii ya ishirini na moja, teknolojia imekuwa uti wa mgongo wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Matumizi ya vifaa vya kidijitali kama vile tarakilishi na simu tambuzi yamebadilisha jinsi tunavyowasiliana, tunavyojifunza na hata tunavyofanya biashara. Hata hivyo, maendeleo haya yanakuja na changamoto zake. Vijana wengi wamejikuta wakitumia muda mwingi kwenye mitandao ya kijamii badala ya kuzingatia masomo yao au kusaidia kazi za nyumbani.

Ni jambo la busara kwa wanafunzi kutumia teknolojia kama nyenzo ya utafiti. Mtandao una hazina kubwa ya maarifa ambayo inaweza kumpa mwanafunzi mwanga zaidi kuhusu mada zinazofundishwa darasani. Badala ya kupoteza muda kwenye michezo ya video isiyo na tija, mwanafunzi anaweza kujiunga na majukwaa ya kielimu yanayotoa mafunzo ya ziada. Wazazi na walimu wana jukumu kubwa la kuwaongoza vijana ili wasitumbukie katika uraibu wa kidijitali ambao unaweza kuathiri afya yao ya kiakili na mahusiano ya kijamii.

Maswali: